**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA**

# TANGAZO

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA ANAWATANGAZIA WANANCHI KUOMBA MKOPO UNAOTOKANA NA ASILIMIA KUMI YA MAPATO YA NDANI USIO NA RIBA.

NAMNA YA KUOMBA:KILA MWOMBAJI AMUONE AFISA MAENDELEO YA JAMII WA KATA ANAYEPATIKANA KATIKA OFISI YA MTENDAJI WA KATA HUSIKA.

MAOMBI YOTE YATATUMWA KWA NJIA YA MTANDAO KWA MKURUGENZI WA JIJI LA MWANZA KUPITIA OFISI YA MTENDAJI WA KATA ULIOPO
KIKUNDI KINATAKIWA KUWA NA SIFA NA NYARAKA ZIFUATAZO:-

1. KATIBA YA KIKUNDI.
2. CHETI CHA USAJILI WA KIKUNDI
3. LESENI YA BIASHARA KWA KIKUNDI CHENYE BIASHARA/VITAMBULISHO VYA UJASIRIAMALI.
4. WANAKIKUNDI WOTE WAWE NA VITAMBULISHO VYA TAIFA
5. TAARIFA YA AKAUNTI KUTOKA KATIKA BENKI ILIYOFUNGULIWA KWA JINA LA KIKUNDI
6. BARUA YA UTAMBULISHO KUTOKA KWA MTENDAJI WA MTAA NA KATA.
7. WANAKIKUNDI WAWE NA SHUGHULI ZA UJASILIAMALI WA PAMOJA.
8. WANAKIKUNDI WASIWE NA AJIRA RASMI
9. VIKUNDI VYA WANAWAKE IDADI YA WANAKIKUNDI NI WATU 5 NAKUENDELEA.
10. VIKUNDI VYA VIJANA IDADI YA WANAKIKUNDI NI WATU 5 NA KUENDELEA NA WAWE NA UMRI KUANZIA MIAKA 18 HADI 35.
11. KIKUNDI CHA WATU WENYE ULEMAVU KIWE NA IDADI ISIYOPUNGUA WATU 2 NA WAWE NA NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA AU HATI YA KIAPO INAYOTHIBITISHA KUZALIWA KWAKE.

MUDA WA MAOMBI YA MKOPO NI KUANZIA TAREHE 15/07/2022.HADI 15/08/2022.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA

SEKIETES YAHAYA
MKURUGENZI HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA